Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Uchunguzi wa fani za lugha zilivyotumika kuibua changamoto za vijana katika riwaya teule za Kiswahili.

**Harrison Onyango Ogutu.**
**Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.**
**Email: harrynamasumbi@gmail.com**

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna mbinu mbalimbali za lugha zilivyotumika kuibua na kudhihirisha changamoto katika jamii. Utafiti huu ulielekezwa na nadharia ya uhalisia ambayo hushughulikia uwasilishi wa uhalisi na ukweli wa mambo katika fasihi. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi huwaweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida, kweli na halisi. Mihimili ya uhalisia iliotumika katika utafiti huu ilikuwa; nguzo ya kielelezo inayosisitiza uigaji wa hali halisi kwa njia ya kweli, wazi na sahihi; nguzo ya matumizi ya lugha ya wakati uliopo na inayosheheni uhalisi na ukweli wa mambo kama yalivyo katika jamii husika ilitumika. Njia kuu ya utafiti huu ilikuwa utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji data. Mbinu ya kithamano ilitumika kuchanganua na kueleza data ya visa na matukio yaliyodhihirisha changamoto dhidi ya vijana. Utafiti huu ulijikita katika muundo wa kimaelezi ambao ni sahili na kueleza mambo yanavyojitokeza kwa uyakinifu. Utafiti huu ulilenga wahusika vijana na changamoto zilizowakabili. Mtafiti alitumia sampuli ya kimaksudi ambapo riwaya alizozifanyia utafiti aliziteua kwa kudhamiria kuwa zilisheheni maudhui mengi yaliyohusu changamoto halisi zilizowakabili vijana katika jamii yao. Data iliyokusanywa ilijumuisha maudhui yenye changamoto halisi zilizowakabili vijana kama vile ufisadi, ubaguzi, umaskini na ukabila. Changamoto hizo zilisababisha athari kama vile kuacha masomo, mimba za mapema, majeraha na vifo. Utafiti huu ulinuia kuwa na natija kwa wasomi, wahakiki na watafiti wa masuala ya lugha na fasihi kwa kuwa sehemu ya kurejelewa. Aidha, matokeo ya utafiti huu yalitoa hamasisho kwa jamii kuhusu changamoto za vijana ili kusaidia kutafuta suluhu kwa changamoto hizo.

**Maneno Muhimu:** Changamoto za vijana, Fani za lugha, Uhalisia.

-------------------------------------------------------------------***-------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA**

Ogutu, H. O. (2021). Uchunguzi wa fani za lugha zilivyotumika kuibua changamoto za vijana katika riwaya teule za Kiswahili. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 3(1), 199-210. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.204



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

**UTANGULIZI**

Vijana katika jamii yoyote ile ni kikundi cha watu kisichoweza kupuuzwa.Viongozi hasa wa kisiasa na hata kijamii wameendelelea kudai kuwa vijana ni viongozi wa kesho. Madai kama haya yatategemea namna ambavyo vijana wanatayarishwa kuongoza kesho. Vijana hukumbwa na kukabiliwa na changamoto nyingi zinazotinga juhudi zao za kuafikia matamanio yao. Kwa miaka mingi imesemekana kuwa vijana ndio viongozi wa kesho, lakini je?, itakuwaje iwapo viongozi hawa wanakabiliwa na matatizo na vikwazo vingi ambavyo huishia kuwanyima fursa za kuongoza kesho?

Mwandishi Ken Walibora ni msanii maarufu wa kazi za kubuni ambaye katika nyingi ya kazi zake ziwe ni Riwaya, Tamthilia au Hadithi Fupi ameshughulikia masuala mengi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Walibora alitumia mbinu kadhaa za kisanaa kama vile vitabiri, virejeshi, taswira, sitiara, tashtiti na ucheshi kutuchorea hali halisi za wanyonge wanyongwao katika mazingira yao wenyewe. Mwandishi kwa kuzingatia uhalisia wa kifasihi aliweza kusawiri ukweli wa hali tata katika jamii kwa kutuchorea migogoro na vita mbalimbali vyenye msingi wake katika uovu wa wanajamii na hasa sana viongozi. Walibora katika kazi zake teule, kwa kuzingatia uhalisia wa kijamii alituchorea changamoto na migogoro iliyowakumba wanajamii wakiwemo vijana. Wahusika vijana ni miongoni mwa wanyonge wengi walionyongwa, ila hawa ni wanyonge ambao hatimaye kama ilivyodhihirika katika Kidagaa Kimemwozea waliamua liwalo liwe. Hatimaye, waliamua kutetea haki yao, kufanya mapinduzi na kuleta mabadiliko lakini kwa tahadhari kuhusu hatari ya hasira, visasi, papara na matumaini ya kupindukia. Senkoro, katika dibaji ya *Kidagaa Kimemwozea* anasema, Walibora kaonyesha tena ufundi wake mkubwa wa kutuchorea hali halisi za wanyonge wanyongwao, tena katika ardhi yao wenyewe ila hawa ni wanyonge ambao hatimaye wanaamua liwalo na liwe. Hata hivyo, si bila tahadhari kuhusu hatari ya hasira, visasi, papara na matumaini ya kupindukia.

Utafiti huu hivyo basi, ulijikita katika utanzu wa riwaya, hususan zile zilizoandikwa na mwandishi Walibora. Riwaya zilizoteuliwa na mtafiti zilikuwa *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi na Kidagaa Kimemwozea.* Katika hizi riwaya, mtafiti alishughulikia suala la changamoto zilizowakabili wahusika vijana kama alivyodhihirisha mwandishi. Kwa misingi hii basi, madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza namna mwandishi wa riwaya teule alivyotumia fani za lugha kuibua maudhui ya changamoto zilizowakabili vijana. Hapa suala muhimu lilikuwa kutathmini namna fani mbalimbali za lugha kama vile jazanda, taswira, methali na zingine zilivyotumika kuibua na kuendeleza maudhui ya changamoto dhidi ya vijana katika jamii. Dhamira ya mwandishi hivyo basi ilikuwa kusawiri hali halisi ya wahusika vijana kwa kuzingatia changamoto na migogoro iliyowakumba katika jamii. Zaidi ya yote, mwandishi anapendekeza utetezi wa haki kwa njia ya amani bila vita na maafa yoyote ili kuleta maendeleo.

Ingawa wahakiki kadhaa walishughulikia riwaya za Walibora huku wakiangazia vipengele mbalimbali vya fani za lugha, suala la jinsi fani za lugha zilivyotumiwa kuibua changamoto zilizowakabili vijana ama kwa hakika halikushughulikiwa. Licha ya kwamba vijana ni muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile, watafiti na wahakiki wa kazi andishi za Walibora hawakuonyesha nafasi hii ya vijana. Hata hivyo, mwandishi Walibora katika riwaya zake aliangazia pakubwa maisha ya vijana pamoja na changamoto zilizowakumba. Hata hivyo, tafiti ambazo zilifanywa katika fasihi hususan kuhusiana na riwaya za Walibora hazikudhihirisha wazi changamoto za vijana na athari zake zilikuwa zipi katika jamii. Vile vile hakuna ithibati ya kuwepo kwa mtafiti aliyechunguza namna



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

ambavyo Walibora alitumia mbinu mbalimbali za lugha kuibua changamoto zilizowakumba vijana. Hivyo basi, ni kwa misingi hiyo ambapo mtafiti alichunguza riwaya teule; *Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi* na *Kidagaa Kimemwozea* ili kujaza pengo hilo.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Kwa mujibu wa uhakiki wa tamthilia ya *Visiki,* Ongeti (1984), mabadiliko mema yaliweza kuwapa watoto na vijana matumaini. Matumaini haya yalipatikana katika elimu. Hata hivyo Ikambili (1997) akihakiki tamthilia hiyo, hakugusia vizingiti vilivyoweza kuzuia vijana kupata elimu ambayo ingefaa kuwapa matumaini ya siku za usoni. Mabadiliko yanaweza kuwepo tu iwapo vijana wameelimishwa na hivyo basi kuleta mageuzi. Haiwezekani vijana kuongoza mwondoko wa mageuzi na mabadiliko pasina elimu. Ingawaje Ikambili (1997) alitambua kuwa elimu ni kichocheo cha mabadiliko, hakuweza kuweka wazi changamoto zilizoweza kuwakabili vijana katika jitihada za kutaka kupata elimu. Hiyo ndiyo sababu utafiti huu ulitofautiana na wa Ikambili kwani mtafiti alimlika changamoto zilizowakabili vijana katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu kama alivyodhihirisha Walibora katika riwaya zake teule.

Ikambili (1997) katika tahakiki ya Visiki anadai kuwa mhusika Amina ni jasiri. Alifikia uamuzi huo bila ya kutuonyesha kijana huyu alikabiliana na changamoto zipi na kuzipiku ili kustahili sifa ya ujasiri. Sifa ya ujasiri ama kwa hakika hutokana na ukweli kwamba mtu hukumbana na majabali mengi ambayo huwa sugu na kwa ukakamavu mkubwa mhusika hukabiliana nayo na hatimaye kuyashinda. Syambu (1997) vile vile hakutuonyesha kwa kina changamoto alizokabiliana nazo mhusika Amina pamoja na athari ya changamoto hizo kwa maisha yake. Mtafiti hivyo basi alilenga kubaini changamoto zilizowakabili vijana pamoja na kuangazia athari zilizotokana na changamoto hizo tofauti na tahakiki alizozifanya Syambo.

Katika tasnifu yake, Kaui (2008), alitusawiria picha ya vijana kwa jumla katika tamthilia alizozitalii. Tafiti hizi kwa jumla zilishabihiana na utafiti huu kwa msingi kuwa zinahusu vijana. Hata hivyo tofauti kuu iliyopo kati ya utafiti huu na hizo nyingine ni kuwa, katika utafiti huu mtafiti alinuia kutalii changamoto halisi zilizowakabili vijana na kutinga juhudi zao za kutaka kuafikia matamanio yao maishani.

Kuhusiana na wahusika katika Riwaya ya Kiswahili, mengi yameandikwa. Mlacha (1985) alichunguza wahusika katika riwaya nchini Tanzania kabla na baada ya miaka ya 1970. Kwa mujibu wake, kabla ya 1970, wanariwaya walitumia sana wahusika miungu, wanyama na watu dhahania kwa kuhofia utawala uliokuwepo ungewaandama, kwa mfano Shabaan Robert, katika *Adili na Nduguze.* Baada ya miaka ya 1970, wasanii walianza kutumia wahusika wa kihalisia kama wakulima na wafanyakazi, kwa mfano *Kiu* na *Nyota ya Rehema.* Utafiti wa Mlacha hivyo basi, uliegemea usawiri wa wahusika kwa jumla ilhali utafiti huu ulichunguza jinsi changamoto zinazowakabili wahusika vijana zilivyojitokeza kupitia fani anuwai za lugha katika katika riwaya teule za Walibora.

Chacha (1986) alihakiki kazi za Kezilihabi katika makala yake "Mazingira ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili" akizingatia riwaya ya *Rosa Mistika.* Alichambua mhusika Rosa katika mazingira ya shule na kutazama ukengeushi. Ingawa Rosa alikuwa kijana katika shule ya upili, mhakiki hakujishughulisha na suala la changamoto dhidi ya kijana huyu katika mazingira yake. Kinyume na uhakiki wa …Chacha, utafiti huu uliangazia udhihirikaji wa changamoto zilizowakabili vijana kupititia fani ainati za lugha.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Akishughulikia ukengeushi wa wasomi katika riwaya za Kezilahabi, Mayaka (1999) aliangalia wahusika wasomi tu bila kujali kama wahusika hao ni watoto, vijana au watu wazima. Kwa njia hiyo hiyo hakuonyesha changamoto halisi dhidi ya wahusika vijana katika mazingira ya masomo. Yeye alijishughulisha sana na usomi na ukengeushi wa wahusika kwa jumla, tofauti na mtazamo wa utafiti huu uliomulika changamoto halisi zinazowakabili vijana katika riwaya teule za Walibora.

Wandera (1996) Akichunguza usawiri wa wahusika wanawake katika ushairi wa Kiswahili (1800-1900), Wandera (1996) aliangazia swala la uhalisia au ugandamizwaji. Alihoji kuwa, kwa mujibu wa mazingira walimosawiriwa ya wakati huo, wanawake walichorwa katika hali yao halisi hata ingawaje ikilinganishwa na miaka ya baadaye inaonekana kuwa mwanamke aligandamizwa. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu ulichunguza namna vijana walivyokumbana na changamoto mbalimbali na kuathiriwa na changamoto hizo katika utanzu wa riwaya teule zilizoandikwa na Walibora. Hata hivyo, ieleweke wazi hapa kuwa utafiti wa Wandera na utafiti huu unahusiana kwa misingi kuwa tafiti hizi mbili zilitumia nadharia ya uhalisia kama msingi wa uhakiki

**MUKHTASARI**

**Uchanganuzi wa Fani za Lugha Zilivyotumika Kuibua Changamoto Dhidi ya Vijana**

**Sitiari/Istiara na Tashbihi**

Ni mbinu ya kulinganisha kitu na kingine, chenye sifa sawa nacho, moja kwa moja bila kutumia vihusishi vilinganishi. Tashbihi ni mbinu ambayo kwayo mtunzi wa kazi ya fasihi hufananisha kitu na kingine kwa njia ya moja kwa moja kwa kutumia maneno kama vile, mithili ya, mfano wa, kama na kadhalika. Sitiari na tashbihi hunuiwa kujenga picha ya mhusika, jambo au kitu kinachozungumziwa.Tashbiha ni ulinganishi wa moja kwa moja kwa kutumia maneno kama vile, mfano wa, sawa na, mithili ya, tamdhili ya, kama, kama vile na kadhalika (Wamitila 2003). Wamitila (2003) vilevile alifafanua sitiari kuwa ulinganishi ambao si wa moja kwa moja; hautambulishwi kwa viungio. Sitiari inapotumika, huwa muhimu katika ujenzi wa taswira katika fasihi. Katika utafiti huu, mtafiti aliweza kubaini baadhi ya sitiari na tashbiha zilizotumika kuonyesha changamoto zinazowakumba vijana.

Vijana Amani na Imani wa *Kidagaa Kimemwozea* walikuwa katika safari kuelekea Sokomoko. Safari hii ni sitiari yenye maana kwamba Imani na Amani walikuwa katika harakati ya kutafuta haki. Kwa mfano, Amani alisafiri kutafuta aliyempoka mswada wake. Ikumbukwe kuwa mswada wa Amani uliibwa na ukachapishwa kama kitabu bila yeye kujua. Kuna mtu aliyemla Jasho Lake. Vile vile Amani alikuwa katika safari ya kutaka kujua ni nani aliyemuua babu yake, Chichiri Hamadi, na kumfunga amu yake, Yusufu. Imani naye alikuwa katika safari ya kutaka kujua ni nani aliyewatuma askari kunyakua shamba la mamake, kumuua mamake na hata kuteketeza nyumba yao akiwa ndani mwa nyumba hiyo. Istiara hiyo ya safari ilidhihirisha dhuluma dhidi ya vijana kama changamoto iliyowakabili.

Kutokana na swala la ubaguzi, ufisadi na ukabila uliokuwa changamoto kubwa kwa vijana, uteuzi wa Mbunge wa Korosho, Bwana Johnstone Mabende kuwa Waziri wa Usalama, ulifananishwa na paka aliyepewa ruhusa ya kulinda kitoweo. Mbunge huyo, aliaminika kuchochea na kufadhili vita vya kikabila katika wilaya ya Korosho. Kijana Jerumani katika *Kufa Kuzikana* aliuliza huku akimrejelea Johnstone Mabende, "Unawezaje kuweka paka kulinda kitoweo?" (uk 163). Hilo la kumteua kiongozi fisadi, mbaguzi na mkabila kama Johnstone Mabende kuwa Waziri wa Usalama wa ndani liliwaudhi vijana. Ufisadi, ukabila na ubaguzi sasa ungepaliliwa na kulindwa kwa



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

nguvu za serikali. Hiyo ilikuwa changamoto kubwa kwa vijana.

**Kinaya na dhihaka**

Kinaya na dhihaka ni mojawapo ya mbinu za lugha zilizotumiwa katika riwaya teule kuonyesha changamoto mbalimbali zinazowakabili vijana. Utafiti huu uliangazia mifano michache iliyodhihirisha hali hiyo. Kwanza, mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea* alionyesha kinaya kwa kumsawiri mhusika Imani akiwa na bashasha na tabasamu huku fundo chungu limemjaa moyoni. Anasema, "Usoni bashasha na tabasamu daima; moyoni fundo chungu, fundo ambalo ni nadra sana kwa watoto wa umri wake kulibeba", (uk 1). Maneno hayo ya mwandishi yalimrejelea kijana mdogo Imani. Ni kinaya kuwa uso wa Imani ulionyesha tabasamu siku zote ila moyoni alikuwa na fundo chungu. Fundo chungu hilo lilisababishwa na changamoto zipi? Baadaye katika uchanganuzi wa mtafiti, ilibainika kuwa changamoto kama vile dhuluma, kifo cha wazazi na umaskini uliomzunguka kijana Imani zilikuwa sababu mojawapo ya kijana huyo kuwa na fundo chungu moyoni.

Ni kinaya kwa zahanati ya Mtemi Nasaba Bora kujulikana kama mahali ambapo watu walikwenda kufia badala ya kupata nafuu. Hali hii ilituonyesha ukosefu wa uwajibikaji wa wahudumu wa zahanati hii na asasi nyingine za kijamii. Si ajabu basi kuona vijana kama vile Bob DJ na Amani walipokosa kuhudumiwa ipasavyo waliishia kutafuta njia mbadala ya matibabu. Mathalani, Bob DJ alipong"atwa na jibwa „Jimmy" aliishia kutibiwa kwa mitishamba na madawa ya kienyeji na rafikiye mmoja. Hivyo ni dhahiri kuwa vijana walikosa huduma muhimu katika asasi za uma kama vile hospitali. Ukosefu wa uajibikaji miongoni mwa wahudumu wa afya ulijitokeza kama changamoto kubwa dhidi ya kijana Bob DJ.

Mtafiti katika utafiti huu alibaini kuwa mbinu ya kinaya ilitumika katika visa mbalimbali kudhihirisha changamoto zilizowakabili vijana. Kwa mfano, katika *Ndoto ya Almasi*, mtafiti aligundua kuwa ni kinaya askari polisi waliotarajiwa kulinda usalama wa wanafunzi wakati wa migomo shuleni, walipogeuka na kuwabaka wasichana wa shule. "Lo! Nilikuwa shule nyingine kukawa mgomo…polisi wakaitwa wakaja kwenye mabweni. Waliwabaka wasichana tele", (uk 102). Kisa hicho cha kubakwa kwa wasichana ni kinyume kabisa na matarajio ya raia kutoka kwa walinda usalama. Kubakwa na kudhulumiwa kimapenzi hasa kwa vijana wasichana ni mmojawapo ya changamoto kubwa ambazo ziliwakabili vijana katika riwaya lengwa.

Pia mtafiti aligundua kuwa ni kinaya kijana Almasi kukwangura alama 35/36 na kukosa nafasi nzuri ya kuendelea na masomo huku mwenzake Roselyne Kinyanjui akipata alama 19/36 na kupata shule nzuri na hata kuhitimu kusomea uanahabari licha ya kutoweza kutamka hata jina lake vizuri. Kwa mujibu wa mwandishi wa *Ndoto ya Almasi,* uk 24, kuna wakati ustahili ulitegemea kilicho mfukoni. Huko kustahili kutegemea kilichoko mfukoni ni hali iliyothibitisha kuwa ufisadi, milungura na hongo vilikuwa vya ushawishi mkubwa. Lakini kwake kijana Almasi ambaye alikuwa maskini hohe hahe hakuwa na namna nyingine yoyote. Alibakia maskini asiyeweza kujiendeleza kimasomo licha ya werevu wake uliompelekea kukwangura alama 35/36. Hata hivyo vijana ambao hawakufanya vizuri katika mitihani lakini wazazi wao walikuwa na uwezo wa kifedha, waliishia vyuo na kuendeleza masomo yao. Kwa jumla basi, ni kinaya waliozaliwa na vipaji kama vile Almasi kutopewa nafasi na badala yake limbukeni kama Roselyne Kinyanjui wasiokuwa na kipawa chochote kupewa nafasi za kazi kutokana na utajiri wa wazazi wao. Kinaya hiki basi kilitumika kuibua umaskini, upendeleo na ufisadi kama



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

ISSN: 2663-9289

changamoto zilizowakabili vijana.

Mtafiti aligundua kuwa mwandishi pia alitumia kinaya kukejeli wakazi wa Soko-mjinga, jijini Tandika, walioacha shughuli zote, wakafunga soko ili kumtahiri mwanamume mmoja aliyekuwa ameepuka kisu cha ngariba. Kulingana na mila na desturi za Wachungwachungwa, tohara kwa wanaume wote lilikuwa jambo la lazima. Mwanamume mmoja katika *Kufa Kuzikana* alieleza,

> …tohara ni jambo la lazima kwa wanaume wote miongoni mwetu sisi Wachungwachungwa… Sisi kumkagua leo, Lo! Kumbe mwenzetu badomtoto" ati. Basi tukaazimia tulifunge soko ili tuigotoe shughuli hii ya dharura kwanza. Wacha mtoto afanywe „mwanamume" ndipo awe na akili, (uk 55).

Maneno hayo ya mwanamume mmoja aliyekuwa kwenye msafara wa watu wengine wengi wakimpeleka mwanamume mwenzao kutahiriwa yalijaa kejeli na dhihaka. Mtafiti alibaini kuwa kule kumuita mwanamume mwenzao „mtoto" kwa misingi kwamba hakuwa ametahiriwa ilikuwa dhihaka kubwa. Ikumbukwe kwamba mwanamume huyo alikuwa baba wa watoto wawili. Hivyo kuitwa „mtoto" kwa mwanamume yeyote, mtu mzima mwenye familia na watoto ni kauli iliyonuia kumkera, kumdharau na kumdhihaki yeyote aliyeepuka kupashwa tohara. Aidha, tendo la watu wote, waume kwa wake kuazimia kufunga soko na kusitisha shughuli zote ili wakampeleke mwanamume asiyetahiriwa atahiriwe ni kinaya kikubwa. Ni kinaya kwa wanaume na wanawke jijini Tandika kuiona shughuli ya kumtahiri huyo mwanamume kuwa ya dharura zaidi na yenye kupewa kipaumbele na uzito kuliko kuendelea kujishughulisha sokoni ili wapate namna ya kujikimu. Ni kinaya kwamba shughuli ya tohara ilipewa umuhimu zaidi kushinda shughuli za kibiashara pale Soko Mjinga. Yaonekana wafanyibiashara wa Soko-Mjinga walikuwa wajinga kiasi cha kutong"amua ni mambo yapi yaliyopaswa kupewa uzito. Visa hivyo, vya kufedhehesha watu hadharani kwa kuwalazimisha kutahiriwa vilikuwa kero na changamoto kubwa kwa vijana. Swala la tohara za lazima kwa vijana wavulana na wasichana lilikuwa changamoto halisi iliyowakumba vijana katika nchi nzima ya Kiwachema. Vijana kama vile Pam, Tim na Akida pamoja na Jerumani waliona mila na desturi hizo kuwa zilizopitwa na wakati. Walikerwa na kuchukizwa sana hasa kutokana na fedheha na madhara mengine ya kiafya yaliyotokana na tohara za lazima. Kinaya hicho kando na kusheheni suala la mila na utamaduni kama changamoto dhidi ya vijana pia kilifumbata dhuluma dhidi ya vijana waliotahiriwa kwa lazima na kuatiriwa pakubwa.

**Chuku**

Mbinu hii hutoa maelezo yaliyotiwa chumvi kwa ajili ya kufanya mambo ya kawaida kuonekana kama ni ya ajabu kupindukia, (Kombo 2013). Chuku ni mbinu ambayo kwayo waandishi hutilia kauli chumvi au hali ya kuongeza habari zisizo za kweli katika maelezo ili kuyafanya yavutie. Katika riwaya teule, *Kidagaa Kimemwozea,* uk 32, kulikuwa na matumizi ya chuku iliyoonyesha changamoto walizokumbana nazo vijana. Kwa mfano, tuliambiwa Amani aliishi na jeshi kubwa la mijipanya". Alichonuia kusisitiza hapa ni ukweli kwamba kijana Amani aliishi maisha ya uchochole, hali yake ilikuwa duni kiasi kwamba hata panya walipata makao katika chumba chake. Yaani kwa mujibu wa mwandishi, umaskini ulikuwa changamoto kubwa iliyomkumba kijana Amani.

Vijana wawili Ben Bella na Mashaka kwa kuzidiwa na hisia za mapenzi kabla ya ndoa waliahidiana kufunga ndoa hata kama watasubiri miaka elfu baadaye, *Kidagaa Kimemwozea,* uk 81. Mapenzi kati ya vijana hawa yalisisitizwa kupitia chuku. Hata hivyo, lazima



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ifahamike kuwa kijana Mashaka alikuwa angali shuleni katika kidato cha tatu, hivyo kujihusisha katika mapenzi kabla ya ndoa ni changamoto iliyobainishwa na mtafiti.

Mwandishi wa riwaya, *Ndoto ya Almasi,* (uk 22) alitumia chuku kubainisha changamoto zilizowakumba vijana. Kwa mfano kijana msichana Nakhumicha alipooleka ilisemekana mapenzi aliyoyapata katika ndoa yake ni makonde na mateke ya usiku na mchana. Yawezekana kwamba Nakhumicha alipigwa na mumewe lakini hilo la „makonde na mateke usiku na mchana" lilitiwa chumvi. Hata hivyo ifahamike hapa kuwa chuku hiyo ilitumika hapa kudhihirisha ukweli kwamba kijana Nakhumicha alikumbana na dhuluma katika ndoa yake. Kuhusiana na suala hilo la ndoa za mapema miongoni mwa vijana katika *Ndoto ya Almasi,* uk 23, mwandishi alitilia chuku alipoeleza kuwa Nekesa na Naliaka, kwa kuhofia kuwa pia wao wangeringwa mimba, waliolewa wakiwa bado hawajui kupenga kamasi puani. Ukweli ni kwamba Nekesa na Naliaka waliozeshwa wakiwa wachanga mno, lakini hilo kutoweza „kupenga kamasi puani" limetiwa chumvi.

Mtafiti vile vile alipata kuwa uraibu wa sigara ulikuwa na madhara mabaya kwa Almasi. Hata hivyo, mwandishi wa *Ndoto ya Almasi* anapotumia Dina kusema, "ananuka (Almasi) vibaya zaidi kama mbwa aliyekufa akaoza", (uk 27), ni chuku tupu. Inasemekana Almasi alinuka kama kitu kilichooza kutokana na uvutaji wake wa sigara. Ifahamike hapa kuwa uraibu wa vileo na mihadarati ni mojawapo ya changamoto ziliwakabili vijana kama ilivyokwishajadiliwa na mtafiti.

**Taswira**

Taswira ni mbinu ambayo picha ya maelezo humjia msomaji kutokana na masimulizi ya mwandishi anaposoma kadhia, Kombo (2013). Mbinu hii ilitumika kuchora picha halisi ya baadhi ya changamoto zilizowakabili vijana katika riwaya teule. Taswira ni picha ambayo humjia mtu akilini anaposoma, kutazama au kusikiliza kazi ya kifasihi. Taswira huweza kufumbata maana fiche ya kijazanda. Taswira huundwa wakati mwingine kutokana na tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, tashhisi, taashira, majazi na chuku. Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya taswira zilizotumiwa na mwandishi zilidhihirisha changamoto na matatizo yaliyowakabili vijana. Baadhi ya taswira hizi ni kama vile, maelezo kuhusu mavazi ya Amani. Licha ya kutubainishia picha ya jinsi alivyovaa, yalisawiri picha ya umaskini. Mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea,* akimrejelea Amani alisema, "Alikuwa kavaa shati la nili lililodondosha vifungo. Suruali yake ya kaki ina viraka viwili vikubwa vya urujuani vilivyochungulia makalioni kama pazia kwenye madirisha ya nyumba", (*uk 1*). Kuhusiana na hali ya umaskini wa Amani, mwandishi anatupa taswira ya makazi ya kijana huyu katika mji wa mwajiri wake. Kibanda cha Amani kinaelezwa kitaswira katika *Kidagaa Kimemwozea*. "Paa la nyasi, sakafu ya vibonde, dirisha la katoni, kitanda cha teremka tukaze, blanketi fupi lenye mianya, jeshi kubwa la mijipanya na mkoba mweusi ukutani", (uk 32). Taswira hiyo ilionyesha kuwa mwajiri hakumdhamini mwajiriwa. Mwajiriwa hapa ni kijana Amani anayedhulumiwa na mwajiri wake Mtemi Nasaba Bora. Hali hiyo mbaya ya maisha ilikuwa changamoto iliyomkabili na kumwathiri kijana Amani.

Hali ya kijana Amani alipotoka hospitalini vilevile ilitupa taswira ya namna kijana huyu alivyokuwa hoi. Inasemekana Amani alipotoka hospitalini alikuwa amekonda na kuwa fremu. Alikuwa na bendeji kichwani, tumboni na sehemu nyingine za mwili. Nguo zake zilimpwaya. Taswira hii pia ilituonyesha athari ya udhalimu na ukatili wa Mtemi Nasaba Bora dhidi ya kijana Amani. Mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea,* alipoeleza hali ya ajira kwa mtemi Nasaba Bora alisema, "Ajira kwa Mtemi Nasaba Bora ilikuwa sawa na kuvuka



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kwa kamba nyembamba ya katani mto usiovukika", (uk 10). Taswira inayojengeka kutokana na maelezo hayo ya kijazanda ni ugumu wa maisha ya wafanyakazi wa Nasaba Bora akiwemo Amani. Si ajabu basi kuona kijana Amani akipitia dhuluma ya kiwango cha juu alipokuwa akifanya kazi kwake Mtemi Nasaba Bora. Ni wazi kuwa kulingana na mtafiti, taswira ni mojawapo ya mbinu alizozitumia mwandishi kwa ufanifu mkubwa kutubainishia changamoto mbalimbali zilizowakabili vijana.

Mtafiti pia alibaini kuwa mwandishi wa *Ndoto ya Almasi* alitumia taswira kuelezea suala la mapenzi ya kimwili miongoni mwa vijana kabla ya ndoa. Vijana wengi wajiingiza katika uasherati na kuhusiana kimapenzi nje ya ndoa. Bila shaka matokeo ya matendo kama haya kama alivyokwisha kueleza mtafiti yalikuwa ni mimba za mapema, kuavya mimba hizo na hata wengine kufariki wakiwa katika harakati za kuavya mimba. Mwandishi alitupa taswira ifuatayo, "Almasi alishangaa, akawa anatokwa tu na majasho mtawalio kama mkimbiaji wa mbio za nyika. Walikuwa wamo katika pilka pilka za kumwamsha aliyelala kitanda kiliposalimu amri wakajikuta sakafuni. Wote waliukosa „uroda" pamoja na kitanda, wakalala sakafuni huku wamenyamaziana kama majabali mawili yaliyokingamana", (uk 28). Ikumbukwe kwamba Almasi na Chebosio walikuwa vijana wadogo wa shule ya upili ambao kwa hakika hawakupaswa kujihusisha na shughuli hii ya uasherati. Hata hivyo, yaonekana vijana hawa walishindwa kujidhibiti wakatawaliwa na kuongozwa na uchu na ashiki za mwili na hatimaye kushiriki ngono wakiwa wangali wachanga.

Kulingana na mtafiti, matakwa ya mila na tamaduni hasa mila zilizopitwa na wakati huwa changamoto kwa vijana. Jamii alimozaliwa kijana Almasi ilisisitiza kutahiriwa hadharani mbele ya watu ili mtu apate heshima ya utu uzima. Si ajabu basi Almasi alipokosa kutahiriwa kimila alifedheheshwa kwa kuvuliwa nguo kadamnasi mbele ya watu. Tendo hili lilikuwa dhuluma kubwa kwa vijana ambao walikuwa wameamua kutahiriwa hospitalini kama alivyofanya kijana Almasi. Mwandishi wa *Ndoto ya Almasi*, (uk 124), alitupa taswira ya mambo yalivyokuwa katika uwanja wa Makutano wakati wa mechi kati ya Bwake FC na Makutano FC. Mwandishi alisawiri hali ambapo kulikuwepo mkurupuko wa watu – watoto kwa watu wazima, wanaume kwa wanawake, wavulana kwa wasichana waking"ang"ania kutazama na kuthibitisha iwapo kweli Almasi alikuwa ametahiriwa baada ya kumvua nguo. Taswira hiyo ilikuwa ithibati kuwa vijana walidhulumiwa kwa msingi ya kutaka kutimiza mila na utamaduni. Tendo la kumvua kijana Almasi suruali hadharani mbele ya umati mkubwa kiasi hicho ni la kuabisha na kufedhehesha sana. Vile vile tendo hilo ni mateso kwa vijana walio na hiari ya kutahiriwa hospitalini au hata kutotahiriwa kabisa.

**Kisengerenyuma**

Amani akiwa kibandani mwake masaa ya alfajiri alikumbuka rafiki yake Fao na kuturudisha nyuma kutusimulia kisa cha Fao kumringa mwanafunzi wake, *Ndoto ya Almasi* (uk 35-37). Mbinu hii ilionyesha jinsi Fao, mwalimu ambaye angali kijana, alivyoshindwa kujidhibiti kuhusiana kimapenzi na mwanafunzi wake. Uasherati na uzinzi wa vijana ulidhihirika kuwa changamoto kubwa dhidi ya ndoto walizokuwa nazo kwani matokeo ni mimba za mapema ambazo zilisababisha vijana wasichana kuwachia masomo njiani. Pia katika hii mbinu rejeshi, usaliti wa viongozi dhidi ya vijana ulianikwa wazi. Ikumbukwe kwamba ni kupitia mbinu hii ambapo tuliarifiwa kuhusu mtoto wa waziri wa mifugo aliyemtunga mimba dadake Fao. Vile vile, ikumbukwe kuwa Fao alikuwa mwalimu na hivyo ilitarajiwa awe mfano wa uongozi bora kwa wanafunzi bali sio kuhusika kimapenzi na wanafunzi wake na hata kumtunga mimba.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Kwingineko ni wazi kupitia mbinu hii rejeshi kuwa asasi za umma kama vile elimu hazikutegemewa sana. Ni katika taasisi za kielimu ambako uovu mwingi ulitokea dhidi ya vijana. Uovu huo na kutotendewa haki ni changamoto kubwa dhidi ya vijana.

Kupitia mbinu rejeshi katika *Ndoto ya Almasi*, kijana Almasi alikumbuka alivyokuwa akirauka alfajiri saa kumi na moja kukamua ng"ombe na kuyapeleka maziwa kwenye lori lililoyapeleka kwenye kiwanda cha K.C.C mjini Kitale. Umaskini wa wazazi wa Almasi haungewaruhusu wamwajiri mfanyakazi wa kukamua ng"ombe, hivyo Almasi alilazimika kutekeleza jukumu hilo kabla ya kwenda shuleni. Almasi alipenda masomo na aliamini kuwa msingi mzuri masomoni ndio siri ya pekee ya kutimiza ndoto zake. Mwandishi alisema;

> Kijana anakumbuka jinsi alivyokuwa anazinduka alfajiri kukamua ng"ombe wao wa gredi na kuyaleta maziwa kwenye ndoo kupimwa uzani na ubora huku akipigwa na kibaridi kikali cha mzizimo, kabla lori kuyachukua hadi kwenye kiwanda cha maziwa cha K.C.C mjini Kitale kuondoka. Anakumbuka jinsi ilivyokuwa sharti akatize au akatiziwe usingizi wake mtamu na ndoto zake za utotoni ili kuliwahi hilo lori lililoondoka mwendo wa saa kumi na moja alfajiri, (uk 3).

Kupitia mbinu rejeshi hapo juu, mtafiti aligundua kuwa kijana Almasi alipitia changamoto ya kuamka asubuhi, kukamua ng"ombe na kupeleka maziwa kwenye lori masaa ya saa kumi na moja alfajiri kukiwa na baridi shadidi. Ilimbidi kijana huyu kufanya hivyo kwani wazazi wake walikuwa wachochole, wasioweza kumwajiri mjakazi. Hivyo basi, mbinu hii ilitumika hapa kuonyesha umaskini wa familia ya Almasi na jinsi ulivyoathiri ari yake ya masomo. Hangeweza kurauka mapema na kujitayarisha kwa masomo badala yake aliamkia kazi sulubu.

Kupitia mbinu rejeshi, kijana Jerumani alimkumbusha Akida (Kipande Madodo) kuhusu vita vya kikabila vilivyozuka wilayani Korosho, eneo la Baraki. Vilevile Jerumani aliyafananisha matukio ya Baraki na mauaji ya halaiki yaliyotokea nchini Rwanda. Halikadhalika swala la unafiki wa viongozi wa kanisa lilijitokeza wazi kupitia mbinu rejeshi katika *Kufa Kuzikana,* (uk 156). Kupitia mbinu hiyo rejeshi, Jerumani alikumbuka vita vya kikabila na athari zake. Pia Jerumani alikumbuka mauaji ya halaiki nchini Rwanda yaliyotokea kwa sababu za kikabila. Hatimaye Jerumani alikumbuka namna ambavyo, makasisi wa makanisa walivyochochea vita vya kikabila na hata kuhusika mmoja kwa mmoja katika mauaji yaliyosababisha vifo vya watu wengi. Ukabila na unafiki wa makasisi ni mojawapo ya changamoto zilizowakumba vijana. Ukabila na unafiki wa dini uliwatamausha vijana na kuwakosesha mengi ya manufaa katika maisha. Ikumbukwe kwamba babake Akida aliuliwa katika vita vya kikabila huku uhusiano kati ya Tim na Pam ukitingwa na sababu za kikabila na ushauri wa kidini. Kijana Akida alikumbuka makala yaliyokuwa na habari kuhusu vita vya kikabila Baraki. Katika makala hayo wafadhili na wachochezi wa vita vya kikabila eneo la Baraki walikuwa wanasiasa na makasisi - viongozi wa kanisa. Madhara ya vita hivyo vya kikabila pia yalionyeshwa. Kwa mujibu wa *Kufa Kuzikana,* (uk 160-161), vita hivyo vilikuwa changamoto kubwa kwa vijana kiasi cha kuwafanya wengi wao kuwa wezi wa mabavu, makahaba, vibaka, ombaomba na wahuni.

**Methali Na Misemo**

Mtafiti alitambua kuwa methali na misemo ilitumika kuibua baadhi ya changamoto zilizowakumba vijana katika riwaya teule. Kwa mfano, kijana Almasi alikosa malezi mema kutoka kwa babake, Mzee Masasi. Mzee



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Masasi hakuwa kielelezo kizuri kwa kijana wake hivyo mwandishi alisema baba mtu alikuwa mvutaji sigara na mlevi wa „kunywa chupa na kifuniko chake", Ndoto *ya Almasi*, (uk 9). Tabia ya Mzee Masasi kuvuta sigara na kunywa chupa na kifuniko chake ni hali ambayo hatimaye kwa njia moja au nyingine ilimwathiri kijana wake Almasi ambaye aliishia kuwa mvutaji sugu wa sigara. Kulingana na mtafiti, misemo „kunywa chupa na kifuniko chake" na „kufungwa mikatale ya utumwa" ilitumika na mwandishi kusisitiza ukweli kwamba vijana wengi waliathirika kutokana na malezi yasiyo mema kwa watoto. Malezi mabaya hasa yale yaliyotokana na tabia zisizo nzuri kutoka kwa wazazi yalikuwa changamoto kwa vijana. Vijana kama Almasi walijipata wameathiriwa na tabia za wazazi wao. Kutowajibika kwa wazazi kama vile mzee Masasi katika malezi kulijitokeza wazi hapa kama changamoto dhidi ya vijana.

Kijana Akida katika *Kufa Kuzikana,* alipojaribu kufuatilia ufadhili wake wa shule ya upili katika ofisi za waziri wa elimu jijini, mhazili wa waziri alimwambia, „Umechelewachelewa ukakuta mwana si wako", (uk 126). Kauli hiyo ya sekretari ilikuwa ithibati kwamba kijana Akida alikuwa keshapoteza ufadhili wake kwa njia ambayo hakuielewa hadi alipogundua kuwa nafasi yake katika shule ya upili ya kitaifa ya Kiwachema, ilikuwa imetwaliwa na mtoto wa tajiri mmoja. Nafasi hiyo ya Akida lazima ilitwaliwa kwa njia za kifisadi hata ingawaje kuchelewa kwa Akida kulitokana na hali yake ya uyatima na umaskini. Mtoto maskini kama yeye, hakuwa na uwezo wa kujitafutia mahitaji ya kimsingi sembuse fedha za masrufu katika shule ya kitaifa. Kijana Akida vile vile alipokuwa akieleza kuhusu hali yao ya umaskini ambao haungewaruhusu kumudu bidhaa muhimu kama vile sukari, maziwa, chumvi, sabuni na mkate alikaulisha kwa methali, „Dau la mnyonge haliendi joshi", (uk 127). Bidhaa kama hizo zilikuwa za watu wenye nafasi kihali. Lakini kwao, Akida, Tim na Tamari, hilo lilikuwa jambo muhali. Umaskini ulikuwa changamoto kubwa kwa vijana hao kiasi cha kutoweza kumudu gharama ya bidhaa hizo muhimu. Hivyo basi, vijana walijizatiti kupata kidogo kupitia kwa vibarua ilmuradi wafanye lolote la halali na wapate chochote cha halali.

**Ucheshi**

Hii ni mbinu ambayo huibua kicheko kwa hadhira. Hadhira hujipata inacheka kutokana na maelezo au mambo wanayoyasikia au kuona. Aghalabu mwandishi anaweza kutumia maneno au kauli za kuchekesha kusema ukweli halisi wa mambo kwa njia ya kuchekesha. Mtafiti alibaini kuwa ucheshi ulitumika kuonyesha mapenzi kati ya kijana Almasi na msichana Chebosio kwa mfano, mazungumzo kati ya Chebosio na Almasi yalijaa ucheshi uliosheheni kauli za mapenzi kabla ya ndoa. Kwa mujibu wa *Ndoto ya Almasi*, Chebosio anasaili, "Kwani unafikiria redio inatangaza sasa kwamba wanaume wote wamekufa duniani?... Najua unataka wafe wote ndipo unipate mimi. Hunipati ng"o!" (uk 137). Kauli hiyo ya Chebosio ilijaa ucheshi uliobeba hisia za mapenzi baina yake na kijana Almasi. Itakumbukwa kwamba kuna wakati Almasi alimleta Chebosio katika chumba chake kula uroda na vile vile hatimaye Almasi alimwoa Chebosio ingawaje kwa hali ya kutatanisha. Maelezo kuhusu mapenzi kati ya Almasi na Chebosio usiku ule Almasi alipomleta Chebosio katika chumba chake pia yalijaa ucheshi. Mwandishi alisema, "Walikuwa wamo katika pilka pilka za kumwamsha aliyelala kitanda kiliposalimu amri wakajikuta sakafuni. Wote waliukosa „uroda" pamoja na kitanda, wakalala sakafuni huku wamenyamaziana kama majabali mawili yanayokingamana", (uk 28). Taswira inayosawiriwa na maelezo hayo hapo juu ni ya kuchekesha. Hata hivyo, la muhimu ni kwamba ucheshi huo unazua suala la mapenzi ya kimwili miongoni mwa vijana ambao bado hawajaingia katika ndoa.


© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Mtafiti aligundua kuwa mwandishi alizungumzia changamoto ya ufisadi dhidi ya vijana kwa namna ya kuchekesha. Majibizano baina ya Mzee Matuko na Sekretari wa kampuni ya Mawakili ya Gembo na wengine yalidhihirisha ucheshi hata ingawa lililokuwa likizungumziwa lilikuwa nyeti. Mzee Matuko akimjibu Sekretari wa Bw Gembo katika *Kufa Kuzikana* alisema; "Kila mtu akija mnamwambia „nenda uje, nenda uje‟…… Mnafikiri nenda uje‟ ni mshumbi wa wali mtu ataula ashibe? Basi tumekula tukashiba „nenda uje‟ hizo mpaka sasa tunazitapika", (uk 46). Matuko alitumia hayo maneno na kauli za kuchekesha kusisitiza ukweli kwamba, walikuwa wamechoshwa na ufisadi wa ofisi ya mawakili ya Bwana Gembo na wengine. Walikuwa tayari kwa lolote ilmuradi walipwe hela zao. Itakumbukwa hapa kuwa kijana Akida alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa wamekuja kudai haki yao. Akida, akiwa pale pamoja na wazee wengine kudai malipo ya bima waliodaikampuni ya mabasi ya „Salama Bus‟. Miaka kumi baada ya kifo cha mamake Akida, hakukuwa na malipo yoyoye hata ingawaje kampuni ya Salama Bus ilidai kuwa ilikuwa ishalipa pesa hizo kupitia kwa kampuni ya Mawakili ya Gembo na wengine. Hivyo basi, kijana Akida alikumbana na ufisadi katika ofisi za mawakili. Akida ni kijana aliyehiniwa haki kwa kuzungushwa huku na huko kwa madai kuwa malipo hayo hayakuwa tayari, sijui faili haipatikani na sababu zingine nyingi.

Mtafiti vilevile kuhusiana na swala la unafiki wa makasisi katika dini, aligundua kuwa lugha ya kuchekesha ilitumika kusisitiza uasherati wa kabila la Wachungwachungwa katika *Kufa Kuzikana,* (uk 200). Tim akimweleza Akida kuhusiana na hatima ya kasisi John Njalala, alisema kuwa baadhi ya waumini walisema kuwa ulokole haukuwa na uwezo wa kuondoa ufuska wa Wachungwachungwa, kabila la kasisi John. Itakumbukwa hapa kuwa uzandiki wa makasisi na viongozi wengine wa kidini ulikuwa tatizo kubwa kwa maisha ya vijana. Vijana kama Tim na Pam waliathirika pakubwa zaidi hasa ikizingatiwa kwamba wao walikuwa walokole na waliochagua njia ya ucha Mungu. Mathalani, Tim aliudhika sana akaamua kuacha dhambi na pia kuacha dini hadi awapate watu walioishi kulingana na walivyohubiri. Ifahamike pia kwamba uzandiki huo wa kidini ndio ulimfanya kasisi John kushiriki katika kufadhili vita vya kikabila eneo la Baraki. Vile vile unafiki huo ndio ulimfanya kasisi John ajiunge na shangaziye Pam kuchongea uchumba kati ya Tim na Pam. Hivyo basi, unafiki wa kidini hata ingawaje uliwasilishwa kwa njia ya kuchekesha, ulikuwa tatizo na changamoto kubwa kwa vijana.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Hata hivyo, kwa mujibu wa mtafiti, sharti vijana wawe tayari kukumbana na changamoto za kila nui katika jamii. Maisha mema ya baadaye kwa vijana yatategemea namna vijana watakavyokabiliana na changamoto za wakati uliopo. Iwapo vijana watatamauka na kushindwa kukabiliana na changamoto zinazoibuka kila uchao, huenda watashindwa kufanikiwa maishani. Vile vile utafiti huu yalithibitisha ukweli kwamba mtunzi wa riwaya lengwa alitumia mbinu mbalimbali za lugha kuibua maudhui mbalimbali yaliyosheheni changamoto zilizowakabili vijana katika riwaya zote tatu. Mbinu hizo za lugha ziligawika katika makundi mawili muhimu, yaani mbinu za kimtindo na mbinu ya kimuundo. Mbinu za kimtindo zilizotumika zilikuwa pamoja na methali, tashbihi, chuku, kinaya na kadhalika. Mbinu ya kimuundo iliyotumika ilikuwa kisengerenyuma au mbinu rejeshi.

**Mapendekezo:** Pia mtafiti anapendekeza waandishi wa kazi za fasihi waandike kazi zao wakifikiria



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.204
Volume: 03 Issue: 01 | Feb-2021|
Received: 01.12.2020; Accepted 05.12.2020; published on 28.02.2021 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H.O., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

manufaa ya kazi hizo kwa wanajamii hasa vijana ambao aghalabu hurejelewa kuwa viongozi wa kesho. Mtafiti anapendekeza kazi za fasihi ziwe na mafunzo katika taasisi kama vile shule na vyuo yanayoweza kuwahami vijana na ujuzi na njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazoibuka kila uchao.

**MAREJELEO**

Chacha, N.C. (1986). Mazingira ya Mwanamke katika fasihi ya Kiswahili; Rosa Mistika wa Kezilahabi Makala katika mwamko vol:3 Chama cha Kiswahili chuo Kikuu cha Nairobi.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Ikambili, H.M. (1997). *Mwongozo wa Visiki.* East African Educational Publishers Ltd. Nairobi.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika.* E.A.P. Arusha.

Kombo, K (2013). *Mwongozo wa Kidagaa Kimemwozea*. Jesma Publishers and Education Boosters Ltd. Nairobi.

Mayaka, G. (1991). Ukengeushi wa wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mlacha, (1985). "*Wahusika katika Riwaya za Kiswahili*" Tanzania 1970-1982 mulika 17. Jarida la TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Ongeti, K. I. (1984). *Visiki.* East African Educational Publishers Ltd, Nairobi.

Shaaban, R (1951). *Adili na Nduguze.* London. Macmillan.

Syambu, B. (1997). *Mwongozo wa Visiki.* Mc Millan Kenya Ltd, Nairobi.

Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana.* Longhorn Kenya Ltd; Barabara ya Funzi, Eneo la Viwandani, Nairobi, Kenya.

Walibora, K. (2006). *Ndoto ya Almasi.* Moran (E.A) Publishers Limited, Judda Comlex, Forest Road, Nairobi, Kenya.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea.*Target Publications Limited, Jengo la Devan, Barabara ya Chiromo, Eneo la Westlands, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi.*Nairobi, Focus publications Ltd.

Wamitila, K. (2003). *Mwongozo wa Walenisi.* Nairobi.Sema sasa Publications,

Wandera, S . P . (1996). " Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: (1800-1900). Uhalisi au Ugandamizaji" Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org